**ANDIKO LA SEPTEMBA YA UTAMBULISHO 2026**

**KUIJENGA AGENDA YA UTAMBULISHO KUWA AJENDA YA KITAIFA**

## 1.0UTANGULIZI

Ndugu zangu waandishi wa habari, nimewaita hapa leo kwa ajili ya kutangaza rasmi Maadhimisho ya Siku ya Utambulisho Duniani, pamoja na kuonesha hatua ambazo Serikali imepiga pamoja na shughuli zitakazotekelezwa nchini katika kipindi cha maadhimisho hayo.

Nchi yetu itaungana na nchi zingine Dunia kuadhimisha siku ya Utambulisho Dunia tarehe 16 Septemba, 2026. Lakini kwa sisi Tanzania kuelekea siku hiyo maadhimisho yameanza leo tarehe 1 Septemba, 2026 kwa shughuli mbalimbali ambazo zitafanyika katika ofisi zote za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) zilizopo katika Wilaya zote Tanzania Bara na Zanzibar.

Tunakwenda katika maadhimisho haya, Tanzania ikiwa ni mwana Majumui wa Afrika, wa Taasisi ya ID4Africa ambayo ilianzishwa tangu mwaka 2014 na kufanya mkutano wake mkuu wa kwanza hapa nchini mwaka 2015. Lengo kuu likiwa ni kuhamasisha nchi za Afrika, kuhakikisha watu wote Afrika wanatambuliwa na kupewa Utambulisho.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) ilianza rasmi zoezi la usajili na utambuzi wa watu nchini kwa ajili ya Kitambulisho cha Taifa Mwaka 2012 kwa kuanza na usajili wa majaribio kwa watumishi wa umma mkoa wa Dar es Salaam. Hatua hii ilikuwa ni utekelezaji wa Sheria ya Usajili na Utambuzi wa watu sura ya 36 ya Mwaka 1986. Kupitia Sheria hii mnamo mwaka 2008 Serikali ilianzisha taasisi inayoshughulikia masuala ya usajili na utambuzi wa watu **“Mamlaka ya**

**Vitambulisho vya Taifa (NIDA)”** kupitia Hati ya Uanzishwaji (Established instrument, 2008) GN 122/2008. Majukumu ya NIDA ni:

i. Kutambua na kusajili watu wanaoishi nchini (Raia, wageni wakazi, wakimbizi na Walowezi) wenye umri wa miaka 18 na kuendelea;
ii. Kutoa Vitambulisho vya Taifa kwa raia, wageni wakaazi, wakimbizi na walowezi wenye umri wa miaka 18 na kuendelea; na
iii. Kutunza Rejesta ya Taifa ya Usajili na Utambuzi wa Watu na kushirikishana taarifa hizo na wadau wengine.

**2.0HALI YA USAJILI NA UTAMBUZI**

Hadi kufikia Julai, 2026 jumla ya watu 27,458,882 wamesajiliwa sawa na asilimia 87.2 ya watu wenye umri wa miaka 18 na kuendelea kulingana na idadi ya watu 31,477,938 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya Vitambulisho 21,526,585 vilizalishwa sawa na asilimia 92.2 ya Namba za Utambulisho 23,344,265 zilizotolewa. Vilevile, jumla ya vitambulisho 20,935,351 viligawiwa kwa wananchi sawa na asilimia 97.2 ya Vitambulisho 21,526,585 vilivyozalishwa.

**3.0ID4AFRICA**

Mwaka 2018, ID4Africa ilianzisha kampeni ya kimataifa ya kuhamasisha Serikali na mamlaka mbalimbali duniani kuitambua tarehe 16 Septemba kuwa Siku ya Utambulisho (Identity Day). **Tarehe 16 Septemba (16.9)** ilichaguliwa mahsusi kuakisi Lengo Na. 16.9 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDG 16.9), linalolenga kuhakikisha upatikanaji wa utambulisho wa kisheria kwa wote, ikiwemo usajili wa vizazi, ifikapo **mwaka 2030.**

Agenda hii inatambua kuwa utambulisho wa kisheria si nyaraka pekee, bali ni miundombinu muhimu ya Taifa inayomwezesha mtu kutambulika kwa usahihi, kupata

huduma na kushiriki katika shughuli za kijamii na kiuchumi. Aidha, unawezesha Serikali kuimarisha usalama, kupanga huduma na rasilimali, na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

JMT ilishiriki kwa mara ya kwanza katika maadhimisho ya Siku ya Utambulisho tarehe 16 Septemba 2025 kama tukio la siku moja. Kwa mwaka 2026, Serikali imepanua wigo wa maadhimisho hayo kutoka tukio la siku moja na kuwa kampeni ya kitaifa ya mwezi mzima wa Septemba yenye lengo ya kujenga uelewa mpana kwa wananchi kuhusu masuala ya usajili na utambuzi na matumizi ya Kitambulisho cha Taifa.

## 4.0 MAADHIMISHO YA SIKU YA UTAMBULISHO, AJENDA YA KITAIFA

Utambulisho wa Taifa haupaswi kutazamwa kama suala la kitambulisho cha taifa (kadi) pekee, bali kama msingi wa kumtambua mtu, kumwezesha kuthibitisha utambulisho wake, kupata haki na huduma, na kushiriki kikamilifu katika uchumi na jamii ya kidijitali.

Kupitia utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhusu mifumo kusomana ili kurahisisha utambuzi wa watu katika utoaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi. Hadi kufikia Agosti, 2026 jumla ya Taasisi **157** ambapo **72** ni za Serikali na **85** ni za Binafsi zimeunganishwa na mfumo wa usajili na utambuzi chini ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

(a) Mfumo huo unaziwezesha Taasisi zilizounganishwa kupata taarifa binafsi za watu ambazo zinatumika kuhakiki, kupunguza au kuondoa vihatarishi vya kughushiwa kwa taarifa binafsi wakati wa kupokea huduma (Identity Authentication and Verification) na hivyo kuboresha utoaji wa huduma za

kiuchumi na kijamii nchini. Taasisi nyingi zimekuwa zikiendesha shughuli na kutoa huduma kwa watu ambao utambulisho wao haujathibitishwa ipasavyo. Hali hii inaweza kuleta changamoto pale inapohitajika kufuatilia taarifa za mhusika au kupata msaada wa Serikali.

Nitoe wito kwa Taasisi za Umma na Binafsi kuunganishwa na Mfumo wa Utambuzi wa NIDA, ili kuhakikisha watu wanaowahudumia wanatambulika na taarifa zao zinathibitishwa kwa usahihi. Hatua hii itasaidia kuimarisha usalama, uwajibikaji na uaminifu katika utoaji wa huduma.

Vilevile, nitumie fursa hii kuwakumbusha wananchi kutotumia Namba zao za Utambulisho wa Taifa (NIN) kuwasajilia watu wengine huduma mbalimbali. NIN ni utambulisho binafsi na inapaswa kutumiwa na mwenye namba husika pekee.

(b) Mfumo huu pia, Kuwezesha Taasisi zinazosimamia masuala ya Ulinzi na Usalama nchini kuweza kudhibiti uhalifu wa kimtandao, ufadhili wa ugaidi na utakatishaji wa fedha kwa kuhakikisha laini za simu zinasajiliwa kwa kutumia Namba ya Kitambulisho cha Taifa (**Jamii Namba**) pamoja na akaunti za benki kufunguliwa kwa kutumia **Jamii Namba**.

(c) Kuwezesha usajili wa walipa kodi kupitia usajili wa Namba ya Mlipa Kodi (TIN) ambapo jumla ya Namba za Utambulisho wa mlipa kodi **milioni 8.4** zimesajiliwa kwa kutumia NINs. Na hivyo kuwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kuongeza wigo wa walipakodi na kurahisisha usimamizi wa masuala ya kodi nchini.

(d) Namba ya Utambulisho wa Taifa imewezesha usajili wa laini za simu **milioni 92,735,799** na hivyo kuondoa udanganyifu na kuimarisha usalama katika mfumo wa mawasiliano nchini.

(e) Kuwawezesha Wazee, Wanawake na Vijana kufungua akaunti na kupata mikopo kutoka katika mabenki na Taasisi za fedha; hivyo kufanikisha utekelezaji wa dhana ya mfumo wa fedha jumuishi (***Financial Inclusion***),

(f) Kuwawezesha wananchi kutambuliwa na kupata huduma za afya kwa urahisi kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF). Kwa sasa, NHIF inatumia Kitambulisho cha Taifa kama njia rasmi ya kumtambua mwanachama anapopata huduma za matibabu. Hatua hii imepunguza gharama kwa serikali ya kutengeneza kadi za Bima ya Afya pamoja kudhibiti udanganyifu kupitia uhakiki kwa kutumia taarifa za NIDA.

(g) Kuwezesha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Tanzania (HESLB) na Zanzibar (ZHELB) katika mchakato wa utoaji mikopo na urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo katika sekta rasmi na zisizo rasmi ndani na nje ya nchi,

(h) Kuwezesha TASAF kufanya uhakiki wa wanufaika kwa kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki hivyo kupunguza gharama za uendeshaji wa mfuko pamoja na kuhakikisha kuwa wanaopata huduma za mfuko ni walengwa,

(i) Kusajili biashara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (PBRA) na kuwezesha kushiriki katika shughuli mbalimbali za biashara pamoja na kusajili miradi ya uwekezaji kupitia Mamlaka ya Uwekezaji na Kanda Maalum za Kiuchumi Tanzania (TISEZA) na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA).

Kwa manufaa haya, itoshe kusema **“UTAMBULISHO NI MSINGI WA HUDUMA, USALAMA, UCHUMI NA MAENDELEO, - UTAMBULISHO WANGU, KIVULI CHANGU.”**

## 5.0SEPTEMBA YA UTAMBULISHO 2026

Kampeni ya kitaifa ya "Septemba ya Utambulisho 2026", itaanza tarehe 1 Septemba 2026, kufikia kilele tarehe 16 Septemba 2026 – Siku ya Utambulisho, na kuendelea hadi tarehe 30 Septemba 2026.

Kampeni itaunganisha

i) Serikali,
ii) Vyombo vya habari,
iii) Taasisi za umma, sekta binafsi na wadau wa maendeleo na
iv) Wananchi katika kuchukua vitambulisho vyao na kuvitumia kwa sahihi.

Kipaumbele kikuu kitakuwa **ugawaji na uchukuaji wa Vitambulisho vya Taifa vilivyokamilika**, huku shughuli za usajili, ufuatiliaji wa Namba za Utambulisho (NINs), marekebisho ya taarifa na elimu kuhusu matumizi ya utambulisho zikiendelea sambamba. Ukweli ni kwamba, safari ya utambulisho haikamiliki kwa mwananchi kusajiliwa au kupata NIN pekee; inakamilika pale utambulisho wake unapomwezesha kupata na kutumia huduma kwa usalama na ufanisi.

## 5.0 UJUMBE MKUU WA KAMPENI KIMATAIFA KWA MWAKA 2026

***"MY IDENTITY, MY SHADOW" - "UTAMBULISHO WANGU, KIVULI CHANGU"***

Kwa upande wa utekelezaji wa kampeni nchini, Serikali inasema: "KIPO? KICHUKUE. KAMILISHA SAFARI YAKO." Ikilenga kuwakumbusha wananchi aidha kuchukua vitambulisho vyao au kukamilisha usajili wao ambao ndio msingi wa kivuli.

## 6.0 KILELE CHA KAMPENI – 16 SEPTEMBA 2026

Tarehe 16 Septemba 2026 itakuwa kilele cha Septemba ya Utambulisho 2026, ikiendana na Siku ya Utambulisho inayohamasishwa kimataifa. Siku hiyo inapendekezwa kutumika kuonesha hatua iliyofikiwa na Tanzania katika kujenga

mfumo wa kisasa, salama na jumuishi wa utambulisho, pamoja na kuzindua toleo jipya la kitambulisho hatua inayolenga kuongeza thamani na matumizi ya utambulisho katika utoaji wa huduma.

Baada ya kilele hicho, shughuli za uhamasishaji, ugawaji wa Vitambulisho vya Taifa na elimu kwa wananchi zitaendelea nchini kote hadi tarehe 30 Septemba 2026.

## 6.0 MIPANGO YA SERIKALI KATIKA KUIMARISHA UTOAJI WA HUDUMA YA UTAMBULISHO NCHINI

Katika kuimarisha utaoji wa huduma za usajili na utambuzi nchini, Serikali inatarajia kutekeleza mipango ifuatayo;

### i. Maboresho ya teknolojia ya kuchapisha vitambulisho

Serikali imeanza kutekeleza maboresho ya teknolojia ya uchapishaji wa vitambulisho kutoka teknolojia inayotumia wino hadi teknolojia ya inayotumia mionzi kuchapisha taarifa katika tabaka (layers) za kitambulisho cha Taifa. Utekelezaji wa maboresho haya utawezesha kuongeza ufanisi katika uchapishaji wa vitambulisho vya Taifa, kuimarisha uimara na usalama wa taarifa zinazochapishwa kwenye vitambulisho, pamoja na kuhakikisha wananchi wanapata vitambulisho vya Taifa vyenye ubora zaidi na kudumu kwa muda mrefu. Aidha, utekelezaji wa mpango huu utaenda sambamba matumizi ya kadighafi mpya za vitambulisho vya Taifa, zenye ubora, uimara na vipengele vya usalama vilivyoboreshwa ili kuinua ubora wa jumla wa vitambulisho vinavyochapishwa.

### ii. Kitambulisho cha Taifa kutumika kuingiza taarifa za mifumo mingine

Serikali inatarajia kuwezesha kadi ya kitambulisho cha Taifa kubeba taarifa za utambulisho wa mtu zilizopo katika vitambulisho vingine ikiwemo bima ya afya, hati ya kusafiria katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, leseni ya udereva na hivyo kupunguza wingi wa vitambulisho kwa mwananchi.

### iii. Usajili wa watu wenye umri chini ya miaka 18

Serikali imepanga kuanza usajili na utambuzi wa watu wenye umri chini ya miaka 18 kwa lengo la kuwapatia **JAMII NAMBA.** Mpango huu utawezesha kila mtu kuwa na namba ya utambulisho wa kipekee kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi tangu kuzaliwa hadi mwisho wa uhai wa maisha ya mtu hapa duniani. Katika kufanikisha hili, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2026/27 Serikali imepanga kufanya majaribio ya usajili wa watoto katika Wilaya ya Wilaya ya Kilolo – Iringa, Rungwe – Mbeya na Kusini – mkoa Kusini. **JAMII NAMBA** itakuwa chachu ya mabadiliko makubwa katika utoaji wa huduma kwa watu wenye umri chini ya miaka 18 ambapo maeneo yote ya utoaji huduma yatahusika ikiwemo katika utoaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu, Bima ya Afya kwa wote, Ujumuishi wa kifedha, kufungua akaunti za benki na usajili wa laini za simu.

### iv. Kuongeza alama za utambuzi katika taarifa za watu

NIDA itaendelea kuboresha Mfumo wa Usajili na Utambuzi kwa kuongeza njia ya alama ya kibaiolojia inayotumia umbile la uso na mboni za macho (Facial and Iris Recognition System). Mfumo huo utawezesha utambuzi wa kibaiolojia kwa wasiokuwa na alama za vidole na kuwezesha kuwatambua kwa usahihi watu wenye umri chini ya miaka 18.

## 7.0 MAMBO MUHIMU YA MSISITIZO

i) Kuitambulisha rasmi Septemba ya Utambulisho 2026 kupitia Mkutano wa Serikali na Waandishi wa Habari tarehe 1 Septemba 2026;

ii) Nitoe mwito kwa wananchi kuchukua Vitambulisho vya Taifa vilivyokamilika na vilivyo tayari kuchukuliwa kwenye Ofisi za NIDA zilizopo katika kila Wilaya, Tanzania Bara na Zanzibar;

iii) Naomba vyombo vya habari nchini kutoa nafasi kwa agenda ya utambulisho katika kipindi chote cha Septemba;

iv) Naomba Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na vitengo vyao vya mawasiliano kushiriki katika kampeni na kutoa elimu kuhusu umuhimu na matumizi ya utambulisho; na

**MWISHO**